# Hadithi 43

# KUJIEBUSHA NA UNAFIKI

Kutoka kwa Abdullah bun Amri, kutoka kwa Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake), amesema:

1. "Mambo manne anaye kuwa nayo anakuwa ni mnafiki halisi, na anayekuwa na moja wapo, anakuwa na sifa ya kinafiki mpaka ayaache;
2. Anapoaminiwa, anafanya hiyana
3. Anapoongea hudanganya
4. Anapoahidi, husaliti
5. Anapokosana na mtu, anavuka mipaka[1]

1 Al-Bukhari (34), na Muslim (58).

## Ayah

Amesema Mola mlezi:

- *﴿Hakika Mwenyezi Mungu anakuamrisheni mzirudishe amana kwa wenyewe. Na mnapo toa hukumu kati ya watu basi mtowe hukumu kwa uadilifu﴾ [An-Nisa: 58].*
- *﴿Hakika wanaafiki watakuwa katika tabaka la chini kabisa Motoni, wala hautowapatia yeyote wa kuwanusuru (145) Isipo kuwa wale walio tubu, na wakatengeneza na wakashikamana na Mwenyezi Mungu, na wakaitakasa Dini yao kwa Mwenyezi Mungu. Basi hao watakuwa pamoja na Waumini. Na Mwenyezi Mungu atawapa Waumini ujira mkubwa﴾ [An-Nisa: 145, 146].*
- *﴿Enyi mlio amini! Timizeni ahadi﴾ [Al-Maaidah: 1].*
- *﴿Enyi mlio amini! Kuweni wasimamizi madhubuti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu mkitoa ushahidi kwa haki. Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na uchamngu﴾ [Al- Maaidah: 8].*
- *﴿Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kuweni pamoja na wakweli﴾ [At-Tawbah: 119].*

## Msimulizi

Ni baba Muhammad, inasemekana ni baba Abdur Rahmaan, Abdullah bin Amri binil A'as bin Waail, kabila la Quraish, ukoo wa Sahmi, alikuwa anajua kuandika kabla hajawa muislam na anajua lugha ya kisiria, alisilimu kabla ya baba yake, alikuwa ni mbora, amehifadhi na msomi, mchana anafunga, usiku anasali. Alimuomba Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) amruhusu aandike hadithi zake, akamruhusu. Alikuwa ni miongoni mwa walio pokea hadithi nyingi kutoka kwa Mtume S.A.W. amefariki mwaka (65H)[1].

## Muhtasari

Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) anataja sifa nne miongoni mwa sifa za wanafiki ambazo haifai kwa mwislam kusifika nazo. Atakae sifika nazo zote, atakuwa ni mnafiki kabisa, na atakae sifika na moja wapo atakuwa amesifika na sifa ya kinafiki, nazo ni; hiyana, uongo, usaliti, na kuvuka mipaka katika ugomvi.

1 Tafsiri yake imehakikiwa katika: "Maarifaat al-Sahaba" na Abu Naim (3/1720), "wa"aliastieab fi maerifat al'ashabi"" cha Ibn Abd al-Bar (3/956), na "Asad al-Ghaba" cha Ibn al.-Atheer (3/245)..

# Ufahamu

Unafiki ni katika maradhi hatari yanayo mpata mtu mmojammoja na jamii kwa ujumla, ndio maana uislam ukatahadharisha sana na kubainisha sifa za wanafiki, ili muumini achukue taahadhari, na ajichunge asije kusifika kwa tabia zao.

1 Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) amewatajia maswahaba zake sifa nne ambazo hasifiki nazo mwislam, bali ni za mnafiki, mtu anapo kuwa nazo zote, anakuwa mnafiki kikamilifu.

Unafiki; ni mtu kudhihirisha kinyume na alicho nacho moyoni, na unagawanyika mara mbili; unafiki wa itikadi; ni mtu kudhihirisha uislam na kuficha ukafiri, huu unamtoa katika uislam. Na hao Mwenyezi Mungu amewasema katika kauli yake: ""Hakika wanafiki watakuwa katika tabaka la chini kabisa Motoni, wala hautowapatia yeyote wa kuwanusuru (145) Isipo kuwa wale walio tubu, na wakatengeneza na wakashikamana na Mwenyezi Mungu, na wakaitakasa Dini yao kwa Mwenyezi Mungu. Basi hao watakuwa pamoja na Waumini. Na Mwenyezi Mungu atakuja wapa Waumini ujira mkubwa" [An-Nisa: 145, 146].". aina nyingine ni unafiki wa matendo; kama uongo na kusaliti, kama ilivyo tajwa kwenye Hadithi. Huu haumtoi mtu katika Uislam, lakini ana kuwa na sifa miongoni mwa sifa za kinafiki, na mwenye nazo anafanana na wanafiki na ameahidiwa adhabu ya Moto[1].

2 Huenda mtu asiwe na hizo sifa nne zote, lakini akawa na sifa moja wapo, atakuwa na kiasi fulani cha unafiki kulingana na jinsi atakavyokuwa ameathirika na sifa hiyo.

3 Sifa ya kwanza: ni kufanya hiyana. Maana ya hiyana; ni kutumia amana kinyume na matakwa ya kisheria; kama kuiuza, au kukanusha kwamba hujakabidhiwa, au kuidharau na kuzembea kuihifadhi. Amana inajumuisha kila alicho aminiwa mtu na kupewa, kama mali au heshima, au haki na zinaweza zikaingia sheria ambazo Mwenyezi Mungu ametupatia kuwa ni amana kwetu, tuzitekeleze na kuzifundisha, ndio maana Mwenyezi Mungu amekiita kitendo cha kwenda kinyume na Qur`ani na mafundisho ya Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) kuwa ni Hiyana: ": "Enyi mlioamini, msimfanyie khiyana Mwenyezi Mungu na Mtume na kuzifanyia khiana amana zenu hali mkijua" [Al-An'fal: 27][2].

4 Sifa ya pili: ni Uongo. Mwenyezi Mungu ameamrisha ukweli na akatuelekeza tuwe wakweli, amesema Mtukufu.: ""Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kuweni pamoja na wakweli" [At-Tawbah: 119].." na Mtume ametahadharisha hatima mbaya ya uongo, akesema: "jiepusheni na uongo kwani uwongo unapelekea katika uovu, na uovu unapelekea

1 Ufafanuzi wa Al-Nawawi juu ya Muslim (2/47).

2 ""Fasihi ya Kinabii"" cha Muhammad Abdul Aziz al-Khouli (uk. 18).

kuingia Motoni, na mtu atasema uongo mpaka aandikwe kwa Mwenyezi Mungu kuwa ni mwongo."[1]". Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) aliona katika ndoto mtu anavuta mdomo wake mpaka kwenye kisogo na kuujeruhi, na pua yake mpaka kwenye kisogo na kulijeruhi na macho yake mpaka kwenye kisogo na kuyajeruhi, akauliza, akaambiwa: ni mtu anaeongea uongo unachukuliwa mpaka unaenea sehemu mbali mbali"[2].

5 Sifa ya tatu: ni kusaliti makubaliaono. Anapo weka ahadi ya makubaliano na mtu anamhadaa kwa kumsaliti. Mwenyezi Mungu ametahadharisha usaliti na ameukataza sehemu zaidi ya moja katika Qur`ani. Amesema Mtukufu: ""Na timizeni ahadi ya Mwenyezi Mungu mnapo ahidi, wala msivunje viapo baada ya kuvithibitisha, ilihali mmekwisha mfanya Mwenyezi Mungu ndiye mdhamini wenu. Hakika Mwenyezi Mungu anayajua myatendayo" [An-Nahl: 91]". Na akesema Mtukufu: Na timizeni ahadi. Kwa hakika ahadi itaulizwa" [Al-Isra: 34]

6 Sifa ya nne: ni mtu kuiacha haki katika ugomvi, na kutumia hila kuirudisha na kujaribu kuchukua ambacho si haki yake, hasa anapokuwa na uwezo wa kuongea na kusimamishaa hoja.

Mwenyezi Mungu amewaamrisha waja wake uadilifu katika kila jambo, na akawazuia wasisukumwe na chuki za ugomvi wakadhulumu upande fulani, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Enyi mlio amini! Kuweni wasimamizi madhubuti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu mkitoa ushahidi kwa haki. Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na uchamngu" [Al- Maaidah: 8]. Na Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) ameeleza hatima mbaya ya anae chukua haki ya mwenzake kwa dhuluma, akasema: "hakika nyinyi mnashtakiana kwangu, huenda baadhi yenu wakawa na ufasaha wa uwasilishaji wa hoja zao kuliko wengine, nikahukumu kuwa ameshinda kwa mujibu wa nilivyo sikia, yeyote ambaye nitampa haki ya mwenzake hata kidogo, basi asiichukue, kwani nitakuwa namkatia sehemu katika Moto"[3] Mambo haya manne yanakusanya misingi ya unafiki, na kuna sifa nyingine ambazo zinatokana na hizi, kama kutotekeleza ahadi[4]. Alama za unafiki na sifa zao ni nyingi, asili yake ni hizo, inatakiwa muislamu ajitahidi asiwe na sifa yoyote katika hizo.

1 Al-Bukhari (6094), na Muslim (2607), kutoka kwa Ibn Masoud.
2 Al-Bukhari (6096), kutoka kwa Samra bin Jundab.
3 Al-Bukhari (2680), na Muslim (1713), kutoka kwa Ummu Salamah, Mungu amuwiye radhi.
4 Al-Bukhari (33), na Muslim (59), kutoka kwa Abu Hurairah.

# Mafunzo

1. Miongoni mwa njia nzuri za Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) za kufundishia, ni kusogeza mukusudio kwa kutumia njia mbali mbali, kama vile idadi. Mwislam anapo sikia kwamba sifa zitakazo tajwa ni nne, anapata hamu ya kuzisikia na kuzikalili hivyo basi. Inatakiwa wasomi na wanao lingania watumie njia kama hizi wakiwa wanazungumza na watu

2. Unafiki ni mbaya sana, na kila sifa yake pia ni mbaya, aliye mkweli na ana anajitambua hujiepusha na sifa hizo na wala hajiaminishimkuwa amesalimika, amesema Ibun abii Mulaikah -miongoni mwa wanafunzi wa maswahaba-: "niliwadiriki maswahaba thelathini wa Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake), wote wanaogopa unafiki usije ukawapata, hayupo anae sema: yeye ana Imani kama ya Jibril na Mikael"(1).

3. Inatakiwa ewe mwenye majukumu, uwe makini na amana unazo kabidhiwa. Sawa sawa kutoka kwa wazazi au wakubwa wako kazini, au marafiki zako, kwa kutumia zaidi kuandika ili usisahau, au usipoteze. Baadhi ya wema walio tangulia walikuwa wakidhibiti kila amana hata kama ni kalamu, au pesa ndogo ya mtoto.

4. Kutekeleza amana ni miongoni mwa sifa nzuri, washirikina katika mji wa Makka walikuwa wakimuita Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) Muaminifu, kwa sababu ni jambo linalo hitaji kujikaza, umakini na kupupia, jitahidi uwe hivyo.

5. Jizoeshe kuwa mkweli hata kama ni katika mambo madogo, tabia ya ukweli ni mazoea, usiseme uongo kwa kisingizio cha mzaha, au kuliwazana, au maslahi, jambo hili halihitaji vitu kama hivyo. Mtu anakuwa na tabia ya uongo mpaka inakita katika damu yake, inakuwa ni kazi kuiacha, kiasi cha kujulikana kwa tabia hiyo katika jamii. Inasimuliwa kwamba Abuu Sufiyaan alitaka kumndanganya Hiraqil kuhusu Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake), lakini aliacha, na alikuwa bado ni kafiri.

6. Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) ameamrisha kutekeleza ahadi hata kama ni kwa washirikina tena katika kipindi cha vita. Hudhaifa bun Yamaan na baba yake, walikuja kwa Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) katika kipandi cha vita ya Badri, wakasema kwamba washirikina waliwachukuwa na kuwauliza, je mnataka kwenda kwa Muhammadi ili mshiriki nae vita?, wakajibu; hapana, sisi tunaenda Madina. Wakachua ahadi ya

1 Al-Bukhari akielezea, Kitabu cha Imani, Sura: Hofu ya Muumini juu ya matendo yake kubatilika bila kujua.

makubaliano kwamba waende Madina na wala wasishiriki vita na Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake). Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) akawambia: “ondokeni, tunatekeleza makubaliano yao, na tunamuomba Mwenyezi Mungu msaada”[1]. Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) hakuwaamrisha washiriki nae vita kuwapiga makafiri kwa ajili ya kutekeleza ahadi

7 Msaliti asifurahi kwa kufaulu, wala matarajio anayoyatarajia kwa usaliti wake, atambue kwamba mwisho wake ni fedheha kubwa. Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) amesema: “kila msaliti anabendera, itasimikwa kwa ajili ya usaliti wake siku ya Kiyama”[2]. Hata kama Msaliti akijua namna ya kupangilia na kuratibu mambo yake, ili asifedheheshwe mbele ya watu, je ataenda wapi siku ya Kiyama na bendera imesimikwa kuonyesha usaliti wake mbele ya viumbe wote?!

8 Usijitafutie sababu ya kufanya hiyana, au uongo , au usaliti, au kuvuka mipaka katika ugomvi, hata kumfanyia aliyekufanyia, tambua kwamba mwislam anafuata maamrisho ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na wala si matamanio yake. Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) amesema: “Tekeleza amana kwa aliye kuamini, na wala usimfanyie hiyana aliye kufanyia hiyana”[3].



**Amesema mshairi:**

*Achana na tabia za watu wasio kuwa na tabia njema***shikamana na tabia za watu bora na wenye adabu*

*Ukiombwa ufanye usaliti au ukiamrishwa***kimbia ujiokoe na moto wa milele.*

**Akasema mwingine:**

*Ukweli anauzoea mkarimu mwenye matarajio ya kukutana na Mwenyezi Mungu*** na uongo anauzoea dhalili aliyefeli.*

*Achana na muongo, na usimfanye kuwa rafiki yako***hakika muongo ni rafiki mbaya.*

1 Muslim (1787).
2 Al-Bukhari (3188) na Muslim (1735).
3 Abu Daawuud (3534).

